Nuru ya Kiswahili, Juzuu 1(2), Desemba 2022: 135 - 163

# Makosa ya Lugha katika Vyombo vya Habari Nchini Tanzania: Uchunguzi wa Televisheni

**Alcheraus R. Mushumbwa**
**Mwanafunzi wa Umahiri, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania**

alche.rwega@yahoo.com

**Ikisiri**
Makala hii inalenga kuchanganua makosa ya lugha kwenye vyombo vya habari nchini Tanzania na kubainisha mbinu za kutatua makosa hayo. Data zilikusanywa kwa mbinu ya hojaji, mahojiano na usomaji wa matini za habari kutoka kwenye chaneli za *TBC1*, *ITV* na *STAR TV*. Nadharia ya Uchanganuzi Makosa imetumiwa kuchambua data na kuwasilisha matokeo ya utafiti. Aidha, utafiti umebaini makosa ya uchanganyaji wa misimbo, matumizi ya maneno yasiyostahili, utenganishaji na uunganishaji wa maneno isivyo, udondoshaji, uchopekaji, matamshi yasiyo sahihi, umoja na wingi, upatanisho wa kisarufi, mpangilio mbaya wa maneno na makosa ya kimantiki. Pia, makala imebaini kuwa makosa hayo yanaweza kutatuliwa kwa kutoa mafunzo ya lugha ya mara kwa mara kwa wanahabari, kutungwa kwa sheria ya kudhibiti matumizi ya lugha, kuhimiza utumiaji wa Kiswahili fasaha, kutumia wanataaluma wa lugha kwenye vyombo vya habari na kufanyika kwa uhariri wa kina. Hitimisho la makala hii ni kwamba makosa ya lugha katika vyombo vya habari nchini Tanzania yanahitaji tafiti nyingi na za kina ili kupata masuluhisho zaidi ya kuyaepuka kwa ustawi wa lugha ya Kiswahili.

**Dhana za Msingi**: Utatuzi, makosa ya lugha, vyombo vya habari, hadhira na lugha fasaha

## Utangulizi

Ufasaha wa lugha ni muhimu katika kuwezesha mawasiliano. Kulingana na BAKITA (2015), ufasaha wa lugha unatokana na kutumia lugha husika kwa usahihi, pasi kuwa na miingiliano ya kimatamshi au matumizi mengine yasiyokubalika. Lugha fasaha ni ile inayokubalika kwa mujibu wa kanuni na ridhaa ya wengi na yenye maneno yanayobeba na kuchukua maana halisi na sahihi. Ni lazima lugha hiyo izingatie taratibu zote za kimatamshi, kimaumbo, kimuundo, kimaana na kimantiki (Bukagile, 2007).Uzingatiaji wa taratibu za lugha huepusha makosa wakati wa kuwasiliana. Kwa hiyo, lugha fasaha inahitajika katika nyanja zote zinazotumia lugha kama nyenzo kuu ya mawasiliano.

Kwa mujibu wa van Dijk (1988), lugha inayopaswa kutumika katika vyombo vya habari, hasa vyombo rasmi ni ile iliyo fasaha tu, inayozingatia maneno sanifu, miundo rasmi na sahihi. Suala la ufasaha wa lugha katika vyombo vya habari limewashughulisha wataalamu mbalimbali kama vile Mwaura (2015), Telg (2015) na Sewangi (2017). Wataalamu hao wanapendekeza kwamba usahihi na usanifu wa lugha ni jambo linalopaswa kupewa kipaumbele kwenye vyombo vya habari kama redio, magazeti, televisheni, tovuti na chaneli za mtandaoni. Kutozingatiwa kwa ufasaha husababisha makosa ya lugha katika vyombo vya habari. Pamoja na mapendekezo ya watafiti mbalimbali, ushahidi bado unaonesha kwamba bado kuna makosa ya lugha kwenye vyombo vya habari katika maeneo mbalimbali ulimwenguni (Akbari na Kheirabadi, 2015; Mugambi, Mukuthuria & Kobia, 2016b). Miongoni mwa makosa ya lugha yanayofanywa mara kwa mara kwenye vyombo vya habari kwa mujibu wa wataalamu hao, ni ukiukaji wa sheria au kanuni za kisarufi, udondoshaji wa maneno na vipashio vingine. Makosa mengine ni utumiaji wa maneno

vibaya au maneno ya mitaani, matamshi yasiyo sahihi, uchanganyaji wa misimbo, uakifishaji, taipolojia na tahajia, matumizi ya lugha isiyo rasmi, utotolojia na mpangilio mbaya wa sentensi (Rowan, 2003; Omoera, 2008a, 2008b; Mozūraitytė, 2015; Hassoon, 2016 na Aditya & Amita, 2017).

Kwa upande wa vyombo vya habari vinavyotumia Kiswahili, makosa mbalimbali ya lugha yanaonekana kufanywa na wanahabari. Makosa hayo ni kama kutumia maneno ya Kiingereza ilihali yapo ya Kiswahili, matumizi mabaya ya msamiati na ukiushi wa sarufi (Mwansoko, 1995; Makunja, 1995; Ponella, 1995 na Kihore, 2004). Pia, makosa mengine ni kutomudu msamiati vizuri, matamshi na tahajia, muundo wa maneno na wiano, wingi na uchache, mpangilio wa maneno kwenye ngeli, tafsiri na utohozi, na matumizi ya sentensi changamano zenye utata (King'ei, 2000; Mukhono, 2008; Jagero, Mohochi na Indede, 2013; Onyango na Odawo, 2016; Mugambi na Wenzake, 2016a, 2016b).

Pamoja na tafiti mbalimbali kuonesha uwapo wa makosa ya lugha kwenye vyombo vya habari vya Kiswahili, bado wanahabari wa Tanzania wanaendelea kufanya makosa mengi ya lugha wakati wa utoaji wa habari. Kwa mfano, Kambaya (2022) anasema kuwa watangazaji wa redio nchini Tanzania hufanya makosa ya kutumia maneno, kuchanganya lugha, udondoshaji na tafsiri sisisi kwa kutaja machache. Hivyo, bado kuna haja ya kuendelea kufanya tafiti mbalimbali zinazochunguza makosa ya lugha kwenye vyombo vya habari na kuyatafutia ufumbuzi kwa ustawi wa lugha adhimu ya Kiswahili. Ikumbukwe kuwa vyombo vya habari vina nguvu kubwa sana katika kushawishi matumizi sahihi na yasiyo sahihi, pamoja na kueneza lugha husika kwa hadhira. Kwa mujibu wa Massamba (1995), vyombo vya habari vina nguvu na ushawishi mkubwa katika kukuza na

kueneza lugha kwa sababu ya uaminifu wake kwa hadhira kwa kuwa yale yanayosemwa katika vyombo vya habari huchukuliwa kuwa ni sahihi. Maelezo haya yanatoa tafsiri kuwa makosa ya lugha yanayotokea kwenye vyombo vya habari yanaweza kuenea kwa hadhira na kuonekana sahihi kwa sababu vyombo vya habari vinaaminiwa na jamii. Ili vyombo vya habari viepuke kueneza lugha isiyo fasaha, tafiti za makosa ya lugha kwenye tasnia hiyo zinahitajika kuendelea kufanywa na wataalamu wa lugha. Kwa ajili ya kutoa mchango katika eneo hilo, makala hii ilichunguza televisheni za *TBC1*, *ITV* na *STAR TV* kwa nia ya kubainisha aina za makosa ya lugha na namna ya kutatua makosa hayo kwa kuzingatia zaidi maoni ya hadhira ya vyombo hivyo vya habari.

**Nadharia ya Utafiti**

Nadharia ya Uchanganuzi Makosa imetumiwa kukusanya na kuwasilisha data. Nadharia hii iliasisiwa na Stephen Pit Corder (1967). Msingi mkubwa wa nadharia hii ni kuchunguza na kuchanganua makosa yanayofanywa na wajifunzaji wa lugha ya pili. Corder anasema kuwa makosa ya lugha yatazamwe kwa faida na kwa umuhimu wake katika mchakato wa kujifunza lugha ya pili kuliko kuchukuliwa kama jambo baya linalotakiwa kurekebishwa/kudhibitiwa. Hii ni kwa sababu makosa hayo hutoa mwanga na uwezo wa mjifunzaji wa lugha ya pili. Baadaye, nadharia hii iliendelezwa na wanaisimu kadhaa. Miongoni mwao ni Gass na Selinker (2008) ambao wanadai kuwa uchanganuzi wa makosa ni aina ya uchambuzi wa kiisimu unaoshughulikia makosa yanayofanywa na wanaojifunza lugha. Grass na Selinker wanapendekeza hatua zifuatazo katika uchanganuzi wa makosa:

(a) Kukusanya data
(b) Kutambua makosa

(c) Kuainisha makosa
(d) Kuonesha mdafao wa makosa
(e) Kufafanua vyanzo vya makosa
(f) Kusahihisha au kutatua makosa

Ijapokuwa nadharia hii hushughulikia zaidi makosa ya ujifunzaji wa lugha, kwa sasa inatumiwa na watafiti kuchanganua makosa yoyote ya lugha katika mawasiliano. Watafiti kama Mugambi na wenzake (2016a, 2016b), Adaku (2016) na Mugambi (2019) wametumia nadharia hii kuchunguza makosa ya kisarufi kwenye vyombo vya habari. Kipengele ambacho kinafaa zaidi katika uchanganuzi wa makosa ni zile hatua zilizopendekezwa na Gass na Selinker (*wameshatajwa*). Hata hivyo, mtafiti hupaswa kuzingatia hatua ambazo zinaendana na malengo ya utafiti wake. Kwa kuzingatia hilo, katika makala hii, tumezingatia hatua nne ambazo ni kukusanya data kutoka kwa watafitiwa na matini za habari, kuchambua data (makosa) zilizokusanywa, kuainisha data (kubainisha aina ya makosa na maoni ya watafitiwa) na kusahihisha makosa (kufafanua hoja za utatuzi wa makosa ya lugha).

**Methodolojia**

Utafiti wa makala hii unahusu vyombo vya habari vya Tanzania kwa kuchunguza televisheni tu. Data zilikusanywa kutoka kwa watafitiwa na kwenye habari zilizoandikwa na kusomwa kwenye vyombo vya habari teule. Mbinu za hojaji, mahojiano, usomaji makini na utazamaji wa habari zilitumika kukusanya data. Mtafiti aliandaa hojaji na kuwapatia watafitiwa ili wazijaze na kisha kumrudishia huku akifanya mahojiano kwa ufafanuzi zaidi. Mbinu hizi zilifaa kutumika ili kupata data kwa muda mfupi na kwa haraka bila kuwachosha na kuwaharibia ratiba watafitiwa. Kupitia hojaji na mahojiano, wasailiwa waliweza kutoa mapendekezo yao kwa uhuru zaidi. Pia, kwa njia ya usomaji makini na utazamaji, mtafiti aliweza kusoma

matini za habari za televisheni zilizoandikwa tovutini na kisha kutazama taarifa za habari kwenye vyombo hivyo.

Sampuli ya watafitiwa 15 na chaneli 3 za televisheni (*TBC1*, *ITV* na *START TV*) iliteuliwa. Mbinu ya uteuzi lengwa ilitumika kuteua sampuli iliyohitajika kwa sababu watafitiwa waliotakiwa ni wale wenye uelewa wa masuala ya lugha tu. Hawa walichaguliwa kwa kigezo cha taaluma ya lugha. Kati ya wasailiwa 15, wasailiwa 2 walihitimu taaluma ya lugha kwa kiwango cha stashahada na wasailiwa 13 walikuwa na shahada ya lugha. Watafitiwa hawa ni hadhira ambayo hutazama, husoma na kusikiliza habari na wana uwezo wa kutambua kama lugha inayotumika ina makosa au la.

Vyombo vya habari vya *TBC1*, *ITV* na *STAR TV* viliteuliwa kwa kigezo cha kuwa na hadhira kubwa kuliko vyombo vingine na vinasikika na kutazamwa maeneo mengi nchini (Media Ownership Monitor Tanzania [MOMT], 2018) pamoja na kutolipiwa ili kupata habari zake. Kwa sababu hiyo, mtafiti aliona ni vizuri kuteua vyombo ambavyo vina hadhira takribani maeneo mengi kuliko vile vyenye hadhira maeneo machache. Idadi ya sampuli ya chaneli za televisheni ilizingatia kanuni ya 10-30% inayopendekezwa na wataalamu wa methodolojia za utafiti kama Kothari (2004) na Ponera (2019). Kwa mujibu wa MOMT (2018:13) idadi ya chaneli za televisheni zinazofuatiliwa sana nchini Tanzania kufikia 2018 zilikuwa 10 ambapo chaneli 3 zilizoteuliwa ni uwakilishi wa 30%.

Data zilikusanywa kutoka kwenye habari za mwaka 2020, kuanzia mwezi Oktoba hadi Novemba. Usanifu auzi elezi ulizingatiwa pamoja na mkabala wa kitaamuli umetumika katika kuchambua data na kuwasilisha matokeo yake. Aidha, madondoo ya data zilizokusanywa kutoka kwa wasailiwa

yamepewa misimbo (MS, 1, 2, 3…) ya kuwatambulisha kulingana na idadi yao.

## Matokeo ya Utafiti

Katika kipengele hiki, makala inawasilisha na kujadili makosa ya lugha yanayofanywa kwenye vyombo vya habari na utatuzi wake kama ambavyo data zimethibitisha. Kipengele kinachofuata ni uchambuzi wa data za makosa ya lugha kutoka kwenye televisheni za *TBC1, ITV* na *STAR TV.*

### Aina za makosa ya lugha katika televisheni za Tanzania

Makosa yaliyojadiliwa hapa, ni yale yaliyokusanywa kutoka kwenye taarifa za habari za televisheni zilizotafitiwa. Mtafiti ameamua kufanya hivyo kwa sababu taarifa ya habari ni kipindi ambacho hutumia mtindo wa lugha rasmi (van Dijk, ameshatajwa). Kulingana na Nadharia ya Uchanganuzi Makosa, mtafiti hupaswa kuonesha kwanza makosa na aina zake kabla ya utatuzi. Hivyo, kipengele hiki kinawasilisha matokeo ya lengo la kwanza la makala hii ambapo aina zifuatazo za makosa zimebainishwa pamoja na mifano yake katika jedwali linalofuata:

**Jedwali: Makosa ya Lugha kwenye Vyombo vya Habari**

| Aina ya Kosa | Mfano wa Makosa na Usahihi |
|---|---|
| Kuchanganya misimbo | Mtihani wa *Form VI* (kidato cha sita), alipiga *stop* (marufuku), *Cement* (saruji) |
| Kutumia neno lisilostahili | *Tujaalie* yaliyojiri (tujuze/tupashe), virusi vya *COVID-19* (Korona), *kusalia* klabuni (kubaki) |
| Kuunganisha na kutenganisha maneno isivyo | a) Kuunganisha maneno: *wanajukumu* (wana jukumu), uzalendo *wakweli* (wa kweli)<br>b) Kutenganisha neno: *zilizo isha* (zilizoisha), *wanao kaidi* (wanaokaidi) |
| Udondoshaji | inaenda vizuri__*sababu* hakuna (kwa), *li_lokuwa* likitokea (lililokuwa), ambao ndio *uli_sababisha* (uliosababisha) |
| Uchopekaji | Virusi *vinavyosababishwa* ugonjwa (vinavyosababisha), *kutoheshimisha* haki(kutoheshimu), wanaumwa *na* ugonjwa (wanaumwa ugonjwa) |
| Matamshi yasiyo sahihi | *Waakti* (wakati), *kumalidhika* (kumalizika), *watakaoudhuria*(watakaohudhuria) |
| Umoja na wingi | *Masaa* (saa), *madhaifu* (udhaifu), *Øjumbe*[1] mbalimbali (ujumbe) |
| Upatanisho wa kisarufi | *Anga ya* kimataifa (anga la kimataifa), *hizi ni mitambo* (hii ni mitambo) |
| Mpangilio mbaya wa maneno | Mapema *hii leo* (leo hii), *kumi na sita elfu* (elfu kumi na sita) |
| Kosa la kimantiki | *Wadhifa uliomstahili* kwa sababu Rose Raponda ni mchumi. (wadhifa aliostahili); Wananchi *wametahadharishwa kutopokea* watu wasiowafahamu (wametahadharishwa kupokea) |

**Chanzo**: Data za Uwandani (2020)

Jedwali linaonesha aina kumi za makosa. Aina hizi zimebainishwa kutoka kwenye makosa 127 ya lugha yaliyokusanywa kutoka katika matini za

[1] Neno 'jumbe' katika makala zilizotafitiwa limetumika kama wingi wa neno 'ujumbe' lenye maana ya taarifa au habari.

habari za televisheni zilizotafitiwa. Kulingana na mawanda ya makala haya, makosa yaliyoainishwa hapa ni yale tu ambayo yalijitokeza mara nyingi zaidi kwenye matini hizo na yatafafanuliwa kwa ufupi kama ifuatavyo:

***Kuchanganya misimbo***

Kuchanganya misimbo ni kosa lililokithiri kwa watumiaji wa lugha ya Kiswahili wanaojua lugha zaidi ya moja wakiwamo wanahabari wa Tanzania. Mwansoko (1995) anasema kuwa ni kasumba ya magazeti ya Tanzania kutumia maneno ya Kiingereza holela ilihali yapo ya Kiswahili. Kwa mujibu wa data iliyokusanywa, wanahabari wanaosoma na kuandika habari katika televisheni zilizotafitiwa huchanganya maneno ya Kiswahili na Kiingereza kwa wakati mmoja wakati wa utoaji wa habari. Mifano inaonesha walitumia maneno "*form VI", "stop*" na "*cement*" badala ya "kidato cha sita", "marufuku" na "saruji." Hili ni kosa kwa sababu dhana zilizoelezwa kwa maneno ya Kiingereza zinaweza kuelezwa vizuri kwa lugha ya Kiswahili kwa sababu kuna maneno ya kutaja dhana hizo. Mifano mingine zaidi ni kama "*electoral votes*" (kura za wajumbe maalumu), "unaweza kuona hiyo *gap…*" (pengo/mwanya), "matibabu ya *utra sound*" (mionzi/radiolojia) na "*Visa* zao" (viza).

***Kutumia neno lisilostahili***

Kwa mujibu wa data iliyopatikana, wanahabari walitumia baadhi ya maneno ambayo hayakupaswa kutumiwa. Mathalani, walitumia maneno "*tujaalie* yaliyojiri", "virusi vya *COVID 19*" na "*kusalia* klabuni" badala ya "tujuze/tupashe", "korona" na "kubaki", mtawalia. Kwa muktadha wa habari, mtangazaji alitaka hadhira ipate taarifa zilizojiri, akasema *tujaalie* badala ya *tujuze/tupashe*; badala ya *kutaja jina la ugonjwa*, anataja *jina la virusi*; na, badala ya kusema kuwa mchezaji *atabaki kuchezea* klabu yake

anasema *atasalia*. Makosa mengine ni kama "filamu ambazo *ziliuza*" (zilipata soko), "kunaweza *kupelekea* jumuiya nyingine kuondoa vikwazo" (kusababisha) na "waandamanaji wameendelea *kutanda* nchini humo" (kutandaa). Matumizi ya maneno yasiyostahili kwenye vyombo vya habari huweza kusababisha athari hasi katika lugha kama kubadili maana halisi ya neno halafu maana hiyo ikawa inatumika kwa kupotosha. Akionesha jinsi ambavyo idhaa za *BBC Swahili* na *DW Kiswahili* zimeshiriki kupotosha maana ya maneno, Shoo (2004) anasema kuwa idhaa hizo zimehusika kwa kiasi kikubwa kutumia neno "mhanga" isivyostahili hadi kupotosha maana yake halisi.

***Kutenganisha na kuunganisha maneno isivyotakiwa***

Baadhi ya matini zilizotafitiwa zilidhihirisha makosa ya uunganishaji na utenganishaji wa maneno. Kwa upande wa uunganishaji, maneno mawili au zaidi yaliyopaswa kutengwa yaliunganishwa kimakosa kama neno moja. Kwa mfano, "*wanajukumu*", "uzalendo *wakweli*" badala ya "wana jukumu" na "uzalendo wa kweli". Kulingana na data hii, kuandika *wanajukumu* na *wakweli* ni kosa kwa kuwa hayo ni maneno tofauti yanayojitegemea wakati wa kuandika. Kwa upande wa kuteganisha neno, baadhi ya matini za habari zilikumbwa na kosa hilo pale ambapo neno moja lilitenganishwa kimakosa kama "*zilizo isha*" na "*wanao kaidi*" badala ya "zilizoisha" na "wanaokaidi". Utafiti umebaini kwamba kosa la utenganishaji wa maneno lilihusu kutenganisha viambishi na mashina ya vitenzi kwa kiasi kikubwa. Hali hiyo inaonesha kuwa waandishi walitatizwa na urefu wa neno hasa wakashindwa kutambua kuwa mashina ya maneno hayo yanapaswa kuunganishwa na viambishi vyake kama neno moja. Kulingana na Aruba (2017), waandishi wanaotenga maneno yasiyopaswa kutengwa huwa wametatizika na urefu wa maneno hayo wakifikiria viambishi na mashina ni maneno

yanyojitegemea. Mifano zaidi ya kosa la kutenganisha neno ni kama "*kwasababu"* (kwa sababu) "*inaidadi*" (ina idadi), "watumishi *wa nne*" (wanne), "*aliye onekana*" (aliyeonekana) na "*lililo leta*" (lililoleta).

***Udondoshaji na uchopekaji wa vipashio***

Data inaonesha kuwa wanahabari hufanya makosa ya uchopekaji na udondoshaji wa vipashio vinavyojenga tungo za matini za habari. Vipashio tofauti (maneno, mofu, silabi) vimedondoshwa kama "inaenda vizuri__*sababu* hakuna", "*li_lokuwa* likitokea" na "ambao ndio *uli_sababisha*" badala ya "kwa sababu", "lililokuwa", "uliosababisha". Kuhusu uchopekaji, matini za habari zilithibitisha kuwa na kosa la uchopekaji wa vipashio (maneno, mofu au silabi) ambavyo havikupaswa kuwa sehemu ya muundo wa tungo husika. Kwa mfano, "virusi *vinavyosababishwa* ugonjwa", "*kutoheshimisha* haki" na "wanaumwa *na* ugonjwa" badala ya "vinavyosababisha", "kutoheshimu", "wanaumwa ugonjwa". Data hii inaonesha kuwa baadhi ya vipashio vya lugha viliingizwa kwenye muundo wa tungo kimakosa. Ilitakiwa kuwa *virusi vinavyosababisha ugojwa* na si *vinavyosababish***wa**, *kutoheshimu* haki na si *kutoheshim***isha**, *wanaumwa ugonjwa* na si *wanaumwa* **na** *ugonjwa*. Mifano migine ya makosa ya udondoshaji na uchopekaji ni "ikiwa ni siku moja __ *kuagiza* wamiliki" (baada ya), "unapaswa *kutole_a* bandarini" (kutolewa), "*walishtumiwa __ kosa hilo*" (kwa), "kipindi *hichi*" (hiki) na "alizotaja kuwa *zinaikabilia* taasisi hiyo" (zinaikabili). Mifano hii inaonesha kuwa baadhi ya vipashio vilivyopaswa kuwa sehemu ya miundo ya tungo hizo vimedondoshwa na vile ambavyo havikutakiwa kuwa sehemu ya miundo ya tungo hizo vimechopekwa kimakosa. Hili ni kosa la lugha kama Ontieri (2015) anavyosema kwamba kosa la udondoshaji au uchopekaji ni hali ya

kuondoa au kuingiza kipashio katika neno kwa njia ambayo inakiuka taratibu za lugha husika.

***Matamshi yasiyo sahihi***

Data ya makala hii inaonesha kuwa wasomaji wa habari walitamka baadhi ya maneno kwa namna ambayo si sahihi. Mathalani, maneno “wakati” na “katika” yalitamkwa “/wa:kti/(waakti)” na “/kalika/(kalika)” badala ya “/wakati/” na “/katika”. Tunaona kuwa katika matamshi haya, sauti /a/ ilivutwa na kuwa sauti ndefu ilihali sivyo inavyopaswa kutamkwa; sauti /t/ ilibadilishwa na kutamkwa /l/ jambo ambalo si sahihi. Mifano mingine ya kosa hili ni kama *“/watakaɔuðuria/ (watakaoudhuria)*, “/*kumaliðika / (kumalidhika)*”, “*/čia/ (chia)”*na “/*tčɛna/ (tchena)*” badala ya “watakaohudhuria/watakaɔhuðuria/”, “kumalizika/kumalizika/”, “cha /ča/” na “tena /tɛna/”. Mbali na data ya makala haya, wachunguzi wengine wa lugha katika vyombo vya habari wanaonesha kuwa makosa ya utamkaji katika vyombo vya habari yanafanywa na wanahabari kila mara (Maina, 2014; Kambaya, 2022). Kwa mfano, Kambaya (keshatajwa) anaonesha kuwa kwa sababu ya athari ya lughamama, baadhi ya wanahabari hukosea kutamka maneno ya Kiswahili kwa ufasaha kama, kutamka “mbu*s*i” badala ya “mbu*z*i”, **“**m*s*ee” badala ya “m*z*ee”, *“s*amani” badala ya “*th*amani”, *“*luga” badala ya “lu*gh*a*”*.

Kulingana na uchunguzi wa makala hii, makosa haya husababishwa na utamkaji wa haraka, athari ya lugha ya kwanza na matatizo ya kimaumbile ya watangazaji. Ikumbukwe kuwa taarifa ya habari inayosomwa mbashara inapaswa kusomwa kwa ufasaha ili ujumbe uliokusudiwa uweze kuwafikia walengwa bila kupotoshwa. Kukosea matamshi kunaondoa muwala na ladha ya habari inayosomwa. Hivyo basi, makala hii inapendekeza

wanahabari kuepuka kusoma habari zao kwa haraka kwa sababu kufanya hivyo kunaharibu utamkaji fasaha na wakati mwingine kupotosha ujumbe na kupoteza ladha ya usomaji. Zaidi, wanahabari wanapaswa kujifunza Kiswahili fasaha na namna ya utamkaji sahihi wa baadhi ya sauti za Kiswahili sanifu zinazowatatiza kutokana na athari ya lughamama.

***Kosa la umoja na wingi***

Matumizi ya vipashio vya umoja na wingi katika maneno ni changamoto inayowakabili wanahabari ambao matini zao zilichunguzwa. Baadhi ya maneno ambayo ni mzizi huru yaliwekwa mofu za wingi au kuondolewa mofu za umoja ili kueleza dhana ya umoja au wingi. Kwa mfano, maneno "saa", "udhaifu", "ujumbe" na "ofisini" yaliandikwa "***ma****saa*", "***ma****dhaifu*", "*jumbe*" na "***ma****ofisini*". Kuweka mofu za wingi au kuondoa mofu ya umoja ili kudokeza dhana za umoja na wingi kwenye maneno hayo, ni kosa kisarufi kwa sababu mizizi ya maneno hayo ni huru na hairuhusu kupokea mofu za umoja au wingi. Kwa mujibu wa Kamusi Kuu ya Kiswahili ya BAKITA (2015) na Kamusi ya Kiswahili Sanifu ya TATAKI (2013), maneno *saa, udhaifu, ujumbe* na *ofisi* hayapokei mofu za umoja au wingi ili kueleza dhana za umoja na wingi. Kosa la namna hii limekuwa likifanywa mara kwa mara na watumiaji wa Kiswahili. Mazoea ya namna hii husababisha kutendeka kwa kosa hili hata kwenye matini ambazo zinatumia lugha rasmi na fasaha. Mbali na mazoea, kutomudu vizuri kanuni za kisarufi ni sababu nyingine ya kufanyika kwa kosa hilo katika matini za habari kwa kuwa wanahabari wengi kwa mujibu wa Kambaya (keshatajwa) hawana umilisi wa kutosha wa sarufi wala taaluma ya lugha.

***Kosa la upatanisho wa kisarufi***

Data inaonesha kuwa wanahabari hawakutumia vema kanuni ya upatanisho wa kisarufi na hivyo kufanya makosa kama "Anga ya kimataifa" na "*hizi ni mitambo*" badala ya "anga la kimataifa" na "hii ni mitambo". Makosa mengine ni "*Shirika la MNH imekuwa bega kwa bega*" (shirika la MNH limekuwa), "*tatizo la kuadimika kwa mafuta imekuwa changamoto* (limekuwa changamoto)". Kwa kutazama data hii, inaonekana wanahabari walitumia viambishi ngeli visivyoendana na nomino zinazotawala kwenye tungo husika na hivyo kufanya kosa la upatanisho wa kisarufi. Ni mumhimu kutambua kuwa upatanisho wa kisarufi ni kijenzi kimojawapo cha ushikamani katika kilongo, inapotokea mofu za upatanisho zikakinzana na nomino inayorejelewa, basi habari itakosa mantiki na wakati mwingine, ujumbe uliokusudiwa unaweza kupotoshwa. Utambuzi wa upatanisho wa kisarufi katika lugha ni suala la kikanuzi, mtu asiyemudu vema kanuni za kisarufi, atafanya kosa la upatanisho bila kutambua kosa hilo. Mifano ya makosa ya upatanisho katika makala hii, inathibitisha kuwa kuna ukosefu wa uelewa wa kanuni za kisarufi kwa wanahabari. Madai kama haya yamewahi kuibuliwa na King'ei (2000) anayesisitiza kuwa kosa la wiano katika vyombo vya habari husababishwa na tatizo la kutomudu kanuni za kisarufi.

***Mpangilio mbaya wa maneno***

Baada ya kuchunguza baadhi ya miundo ya tungo za matini zilizotafitiwa, ilibainika kuwa tungo hizo zilikiuka miundo sahihi ya Kiswahili. Kwa kawaida, katika Kiswahili, kivumishi hutakiwa kufuata nomino lakini baadhi ya miundo ilikuwa kinyume na kanuni hiyo. Kwa mfano, *"mapema hii leo*" na "*kumi na sita elfu*" badala ya "mapema leo hii" na "elfu kumi na sita". Mifano hii inaonesha kuwa vivumishi vimetangulia nomino zinazopaswa kuvumishwa. Hali hii husababishwa na uzungumzaji wa

mazoea, kutomudu vema kanuni za mpangilio wa tungo na athari ya muundo wa lugha ya Kiingereza (Kambaya, 2022). Mifano mingine zaidi ni kama "*Moscow hivi majuzi*" (hivi majuzi, Moscow), "*Bwana Kenyatta aidha*" (aidha, Bwana Kenyatta). Kosa la mpangilio katika tungo hizi limetokana na kutofuata matumizi sahihi ya viakifishi pamoja na kutozingatia muwala katika matini.

***Kosa la kimantiki***

Ukosefu wa mantiki katika matini za habari ni kosa lingine linalokumba vyombo vya habari kama ambavyo utafiti wa makala hii umebaini. Mifano ifuatayo inathibitisha hilo kupitia data kama vile "***Wadhifa uliomstahili*** *kwa sababu Rose Raponda ni mchumi*" (wadhifa aliostahili); "*wananchi* ***wametahadharishwa kutopokea*** watu wasiowafahamu" (wametahadharishwa kupokea). Vifungu hivi vya maneno havileti mantiki kwa hadhira kwa sababu mtu ndiye anayestahili kupewa wadhifa na sio wadhifa kumstahili yeye. Pia, matumizi ya maneno "tahadharishwa" na kikanushi "kutopokea" kwa pamoja yanavuruga kabisa mantiki ya kifungu cha habari. Ikiwa wananchi walitahadharishwa kupokea watu wasiowajua, maana yake walipewa hadhari juu ya upokeaji wa watu hao na si kutowapokea. Mifano hii inathibitisha kuwa wanahabari hufanya makosa ya kimantiki katika kuwasilisha habari zao; jambo ambalo linaweza kupotosha maudhui ya habari yaliyokusudiwa. Kulingana na Odeo na Geoffery (2008), makosa ya kimantiki katika mawasiliano hutokana na upotofu wa mawazo au mpangilio wa maneno kwenye sentensi na hutokea wakati watu wanapozungumza au kuandika kwa kasi sana. Hivyo, ni muhimu kwa wanahabari kuwa makini katika uandishi au usomaji wa habari ili kuepuka kufanya kamosa ya kimantiki ambayo yanaweza kuvuruga ujumbe unaokusudiwa kufikishwa kwa hadhira.

Hadi kufikia hapa, makala imechambua makosa ya lugha kwa mujibu wa data ya utafiti iliyokusanywa na kubainisha aina kumi za makosa kama jedwali linavyoonesha. Makala inasisitiza kuwa makosa hayo ni yale yaliyokusanywa kutoka kwenye habari zilizosomwa na kusikilizwa na mtafiti. Kipengele kinachofuata kinajadili utatuzi wa makosa ya lugha yanayofanyika kwenye vyombo vya habari vya Tanzania kutokana na data iliyokusanywa kwa ajili ya kipengele hicho.

## Utatuzi wa makosa ya lugha kwenye vyombo vya habari nchini Tanzania

Utafiti wa makala hii ulilenga pia kubainisha hatua za kuchukuliwa ili kuepuka makosa ya lugha katika vyombo vya habari vya Tanzania kutoka kwa hadhira ya televisheni za *TBC1*, *ITV* na *STAR TV*. Mapendekezo yafuatayo yalipatikana kutoka kwenye data iliyokusanywa kwa mujibu wa hadhira ya vyombo vya habari vilivyotafitiwa:

(a) Kutolewa kwa mafunzo ya matumizi ya lugha fasaha
(b) Kutungwa kwa sheria za matumizi ya lugha fasaha
(c) Kuhimiza matumizi ya Kiswahili fasaha
(d) Vyombo vya habari kutumia wanataaluma wa lugha
(e) Wanahabari kuwa na taaluma ya lugha
(f) Kufanya uhariri wa kina kabla ya kutoa habari

### *Kutolewa kwa mafunzo ya matumizi ya lugha fasaha*

Hoja iliyotajwa na kuelezwa kwa wingi na watafitiwa ni kutoa mafunzo juu ya matumizi ya lugha fasaha kwenye vyombo vya habari. Msingi wa hoja hii ni kwamba vyombo vya habari, kwa kushirikiana na wataalamu wa lugha kupitia taasisi zenye mamlaka ya kusimamia lugha ya Kiswahili, lazima vitoe mafunzo ya mara kwa mara kwa wanahabari juu ya matumizi ya lugha fasaha. Kwa mujibu wa watafitiwa, utoaji wa mafunzo ya

matumizi sahihi ya lugha kwa wanahabari ni njia mojawapo ya kutatua makosa ya lugha yanayofanyika katika vyombo vya habari vya Tanzania. Katika kulijadili pendekezo hili, mtafitiwa mmojawapo alisema: "Kuwepo na warsha/makongamano yanayohimiza matumizi sahihi ya lugha katika vyombo vya habari" (MS3). Mtafitiwa mwingine naye alitoa maoni kuwa: "Serikali, kwa kushirikiana na Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), iendelee kutoa mafunzo, warsha na semina mbalimbali kuhusu matumizi sahihi ya Kiswahili" (MS13).

Maoni ya watafitiwa hawa yanatafsirika kuwa wanahabari hufanya makosa ya lugha kwa kukosa maarifa ya matumizi sahihi ya lugha. Hivyo, kuendelea kutoa mafunzo ya matumizi sahihi ya lugha, umuhimu wa kutumia lugha fasaha kupitia semina au warsha, mafunzo ya muda mfupi na makongamano ya lugha, kutasaidia kurekebisha makosa hayo. Kulingana na maoni ya Mugambi na wenzake (2016b) na Omoera (2008a), wanahabari wanapaswa kupewa semina na mafunzo ya mara kwa mara juu ya lugha fasaha.

***Kutungwa kwa sheria za matumizi ya lugha fasaha***

Pendekezo lingine la utatuzi wa makosa ya lugha kwenye vyombo vya habari vya Tanzania ni uwapo wa sheria za matumizi ya lugha fasaha. Watafitiwa walifafanua kuwa kuna ulazima wa kutunga sheria kali za kudhibiti matumizi ya lugha yenye makosa ya kila mara. Baadhi ya mapendekezo hayo yalikuwa: "Kanuni na taratibu za kisheria ziwekwe ili kuweza kuondokana na tatizo la matumizi yasiyo sahihi katika lugha pindi vyombo vya habari vinapotoa matangazo kwa lugha ya Kiswahili" (MS6). Naye mtafitiwa mwingine alisema, "Taasisi zinazosimamia mawasiliano na habari ziweke kanuni zinazowabana waandishi kutumia lugha inayofaa

kulingana na muktadha wa mawasiliano" (MS15). Maoni haya yanamaanisha kuwa hadhira inaamini kutungwa kwa sheria au kanuni zinazoongoza matumizi sahihi ya lugha kwenye vyombo vya habari kutasaidia kupunguza makosa ya lugha. Msingi wa suluhisho hili unatokana na imani kwamba baadhi ya wanahabari hufanya makosa ya lugha kwa makusudi au mazoea. Akifafanua zaidi juu ya utungwaji wa kanuni za kutumia lugha fasaha, mtafitiwa mmojawapo alisema:

> "Wanahabari wengi hufanya makosa ya maksudi au holela wakidhani kufanya hivyo ni kuleta ladha au ubunifu mpya kwenye utangazaji wao. Wakati mwingine, wanahabari huhisi kwamba kufanya hivyo ni kuwa na mtindo wa lugha unaowavutia au kuwafurahisha wasikilizaji au watazamaji wa vyombo hivyo. Hivyo, ili kuondoa kasumba hiyo, ni lazima mamlaka husika zitunge sheria za kuwabana na anayekiuka aadhibiwe" (MS14).

Data hii ni mfano mmojawapo wa uhalisi wa matumizi ya lugha katika jamii ya Watanzania, hasa kwenye muktadha wa vyombo ya habari. Kauli zenye ukiushi wa upatanisho wa kisarufi, uchanganyaji wa misimbo (Kiswahili na Kiingereza), maneno yasiyo sanifu na ya mitaani, husikika mara nyingi kwenye vipindi vya redio na televisheni kutoka kwa watangazaji kama data ya makosa inavyodhibitisha uwapo wa kosa la upatanisho wa kisarufi, wingi/umoja na matumizi ya maneno yasiyo sahihi. Hivyo, ili hali kama hii idhibitiwe na kufanya wanahabari kujua kuwa hayo ni makosa, kuna haja ya kutungwa sheria au kanuni zinazozuia matumizi ya lugha isiyo fasaha. Simba (1995:63) akijadili umuhimu wa kuwa na sera katika idhaa za Kiswahili, ana maoni sawa na ya watafitiwa wa makala hii anaposema kwamba:

> Kwa hivyo kutokana na baadhi ya matatizo haya niliyoyataja hapana shaka ipo haja kubwa ya vyombo vyetu vya habari vinavyotangaza kwa lugha hii ya Kiswahili kuwa na sera, sera ambayo itafuatwa na idhaa kadhaa kama si zote ya kudhibiti matumizi mazuri ya maneno ya Kiswahili, kwa kuzuia, kukataza au kusahihisha matumizi yote mabaya ya maneno ya Kiswahili ambayo yanaweza kuleta utatanishi wa maana kwa wasikilizaji wa idhaa hizi za Kiswahili. Haja ya kuweka sera katika matumizi ya Kiswahili katika vyombo vya habari ipo, na ipo kwa misingi ya kuvifanya vyombo vinavyotumia lugha hii kutumia lugha iliyo nzuri na inayokubalika au tuseme Kiswahili sanifu na fasaha.

Mtazamo wa namna hii unaungwa mkono na baadhi ya watumiaji wa Kiswahili na wale wanaopenda kulinda hadhi ya lugha hiyo. Mathalani, aliyekuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Hassan Suluhu (sasa ni Rais), akiwa mgeni rasmi katika maadhimisho ya siku ya Kiswahili yaliyofanyika Jijini Dodoma, tarehe 20 Januari, 2021, alionesha kukerwa na matumizi ya neno ***kwio*** katika Kiswahili na kuzitaka mamlaka zinazosimamia Kiswahili ziweke mikakati ya kudhibiti matumizi ya maneno yasiyo sanifu katika Kiswahili.

***Kuhimiza matumizi ya Kiswahili fasaha kwenye vyombo vya habari***

Uhimizaji wa matumizi ya lugha fasaha katika vyombo vya habari vya Tanzania ni jambo ambalo utafiti huu umelibaini kama suluhisho la makosa ya lugha. Watafitiwa walikiri kuwa, bila kuhimiza matumizi sahihi ya Kiswahili, makosa ya lugha yataendelea kushuhudiwa kwenye vyombo vya habari. Ithibati mojawapo ya hoja hii ni baadhi ya majibu ya watafitiwa yaliyosema, “Watu wa televisheni watumie msamiati wa Kiswahili kwa ufasaha ili kuongeza idadi ya wafuatiliaji” na “wahariri watilie mkazo matumizi sahihi ya Kiswahili sanifu” (MS2 na MS14). Katika mifano hii, MS2 anasisitiza na kupendekeza kuwa matumizi ya msamiati wa Kiswahili

fasaha katika vyombo vya habari yatasaidia kutatua makosa ya lugha. Imani yake ni kwamba kufanya hivyo kutavutia hadhira kufuatilia vyombo hivyo. Kwa upande mwingine, MS14 anaona kuwa wahariri wa vyombo vya habari wanapaswa kuhimiza matumizi ya Kiswahili sanifu. Hoja ya MS14 ina mantiki kubwa kwani, katika chombo chochote cha habari, habari haitolewi kabla ya kuhaririwa. Hivyo, wahariri wakihimiza waandishi na watangazaji kutumia Kiswahili fasaha, ni wazi kuwa makosa ya lugha yatapungua au kuepukwa kwa kiwango chake. Pia, ikiwa watumiaji wa Kiswahili watahimiza matumizi ya lugha fasaha, basi vyombo vya habari vitazingatia matumizi sahihi ya lugha.

Jambo hili linawahitaji wadau wote wa lugha, wanahabari wenyewe, hadhira na watalaamu wa lugha kushirikiana. Mbinu zinazoweza kutumiwa ni kuendelea kutoa elimu juu ya makosa ya lugha kupitia semina na warsha mbalimbali. Pia, kutoa machapisho ya mara kwa mara juu ya matumizi sahihi ya lugha, makosa ya kisarufi na uandishi unaofuata lugha sanifu na fasaha. Kwa mfano, BAKITA limekuwa likitoa machapisho mbalimbali, makala kupitia gazeti la *Habari Leo* na vipindi vya Kiswahili kupitia *Radio One*. Aidha, wanataaluma wa Kiswahili wamekuwa wakisisitiza matumizi sahihi ya lugha (Kanuri, 1995; Maina, 2013; Sewangi, 2017 na Sigalla, 2019). Kwa upande mwingine, hadhira ya vyombo vya habari ambayo ina uelewa wa masuala ya lugha, inayokerwa na lugha isiyo fasaha au makosa ya mara kwa mara kwenye vyombo vya habari, inaweza kusisitiza matumizi sahihi ya lugha kwa kuvikumbusha vyombo vya habari pindi vinapokosea. Baadhi ya hadhira huviandikia vyombo vya habari kuvitaka kuacha kufanya makosa ya lugha ya mara kwa mara, kuyasahihisha na kudumisha lugha fasaha (Shoo, 2004 & Mwaura, 2015). Hivyo, ni maoni ya makala hii kuwa

mbinu hii inafaa kusaidia kutatua tatizo la makosa ya lugha kwenye vyombo vya habari nchini Tanzania.

***Vyombo vya habari kutumia wataalamu wa lugha***

Wataalamu wa lugha ni watu wenye umahiri wa masuala ya lugha. Wanamudu vema kanuni na miongozo ya utumiaji wa lugha kwa kuzingatia miktadha ya matumizi. Hawa wanajua kuwa, makosa ya lugha yasipodhibitiwa, huharibu lugha. Wanajua na kufahamu umuhimu wa kutumia lugha fasaha na wako tayari kujirekebisha au kurekebisha makosa ya lugha. Wataalamu wa lugha wanafaa kutumiwa na vyombo vya habari ili kusaidia kutatua matatizo ya makosa ya lugha katika vyombo hivyo. Mbinu hii ilielezwa kufaa katika kutatua makosa ya lugha kwenye vyombo vya habari. Msisitizo unawekwa kwa vyombo vya habari vya Tanzania kutumia wataalamu wa lugha ili kusaidia kuepuka makosa ya lugha. Baadhi ya watafitiwa walitaja mbinu hii kama suluhisho kwa kusema yafuatayo: "Runinga zinapaswa kuwatumia wasomi au wajuzi wa lugha katika matangazo ili kuepusha makosa ya lugha" (MS9) na "vyombo vya habari vitumie wataalamu wa lugha katika kueleza istilahi sanifu za Kiswahili kwa dhana za kisayansi na teknolojia" (MS10). Kwa mujibu wa makala hii, hadhira inavitaka vyombo vya habari kutumia wanaisimu ili kusaidia kurekebisha makosa ya lugha kwenye vyombo vya habari. Kwa kuwa kuna makosa ambayo hufanywa na wanahabari kwa kutojua kanuni za lugha. Hivyo, ni muhimu vyombo hivyo kuwa na wanaisimu watakaoelekeza matumizi sahihi ya lugha. Kuna umuhimu pia kwa vyombo vya habari kuajiri wahariri waliosomea isimu ambao kazi yao itakuwa ni kusaidia kuelekeza matumizi sahihi ya lugha (Gbara, 2001). Wahariri hao watasaidia kukosoa lugha iliyotumika, kubainisha na kusahihisha makosa ya lugha yanayojitokeza katika habari kabla hazijatolewa au kuwasaidia wanahabari

kubaini makosa wanayofanya wakati wa utangazaji ili kuyarekebisha. Ni maoni ya makala hii kwamba mbinu hii ni mwafaka zaidi kwani hufanyika, si tu katika vyombo vya habari, bali hata katika maandiko ya kitaaluma na nyanja nyingine zinazotumia lugha fasaha.

***Wanahabari kuwa na taaluma ya lugha***

Taaluma ni elimu inayopatikana kwa kujifunza au kufundishwa (TATAKI, 2013). Hivyo, taaluma ya lugha ni elimu inayohusu masuala ya lugha. Mtu mwenye taaluma au mtaalamu wa lugha ni mtu aliyesomea masuala ya lugha na kufuzu. Mtu wa namna hii ni mjuzi wa lugha ambaye anajua kwa kiwango kikubwa matumizi sahihi ya lugha na kwa ufasaha. Hata pale anapokosea, kwa sababu ya utaalamu wake, inamuwia rahisi kutambua makosa na kuyarekebisha. Watafitiwa waliona kuna umuhimu wa wanahabari kupata taaluma ya lugha (Kiswahili) ili kuwasaidia kutofanya makosa ya lugha. Baadhi ya watafitiwa walisema: "Watangazaji wawe wataalamu wa lugha pia na ufaulu mzuri wa lugha ya Kiswahili kiwe kigezo cha kuajiriwa" (MS12). Mtafitiwa mwingine alifafanua hoja hii kuwa, "Katika vyuo vinavyotoa astashahada, stashahada, shahada, shahada ya uzamili na shahada ya uzamivu, wanahabari wapewe mafunzo yanayohusu sarufi ya Kiswahili na matumizi yake ili wawe bora watakapopata fursa ya kuwa watangazaji na waandishi" (MS15).

Kulingana na data, imethibitika kuwa njia mojawapo ya kupunguza au kuzuia makosa ya lugha kwenye vyombo vya habari ni kuwa na wanahabari wenye elimu ya lugha. Massamba (1995:7) anashauri kwamba, mtu anapoandika habari katika gazeti, lugha yake sharti ioane na mada na muktadha wa habari yenyewe; pale ambapo Kiswahili sanifu kinatakiwa sharti kitumike. Kwa mujibu wa Massamba, hayo yote yanawezekana tu

iwapo mwanahabari amepata mafunzo kamili ya lugha. Anasisitiza zaidi kuwa, ili vyombo vya habari viweze kukidhi haja ya kukikuza Kiswahili, kukiendeleza na kukieneza, kuna haja ya kuwa na wataalamu ambao, sio tu kwamba wamesomea utaalamu wa uandishi wa habari na utangazaji, bali pia ni mahiri wa upeo wa juu wa Kiswahili (Massamba, ameshatajawa). Gbara (2001) akijikita katika Kiingereza, anashadidia hoja hii akisema kuwa kuna ulazima wa kufundisha somo la sarufi ya lugha katika vyuo vya uandishi wa habari ili kutatua tatizo la makosa ya kisarufi yanayofanywa na wanahabari.

***Kufanya uhariri wa kina wa habari***

Kuhariri ni kusoma maandishi na kuyasahihisha, kuyarekebisha na kuyapanga katika utaratibu unaofaa kwa ajili ya kuchapa katika gazeti, kitabu au jarida (TATAKI, 2013; BAKITA, 2015). Mintarafu ya fasili hii, kazi yoyote ya maandishi au ya mazungumzo yaliyorekodiwa katika mahojiano na vipindi mbalimbali vya redio na televisheni isipohaririwa, itakuwa na makosa mbalimbali. Ili kurekebisha makosa hayo, ni lazima kufanyike zoezi la kuhariri habari na matangazo yote yanayotolewa katika vyombo vya habari. Uhariri wa namna hiyo ni lazima uwe wa makini na wa kina zaidi. Wakipendekeza njia hii, baadhi ya watafitiwa walisema: "Televisheni ziajiri wahariri wa taarifa au matangazo ili kupitia habari au tangazo kabla ya kurushwa au kutangazwa." (MS1) na "Habari ihaririwe na wataalamu wa lugha kabla haijatangazwa/haijasomwa" (MS12). Tafsiri inayopatikana hapa ni kuwa kuhariri habari na matangazo kabla ya kurushwa hewani ni muhimu sana katika kuepuka kutoa habari zenye makosa ya lugha.

Kwa mujibu wa Massamba (1995), Omoera (2008b), Mwaura (2015), Mugambi na wenzake (2016a), makosa mengine ya lugha katika vyombo vya habari husababishwa na kutofanyika kwa uhariri wa kina. Mukhwana na Mukhwana (2017) wanasisitiza kuwa baadhi ya matini za habari huwa na makosa yanayosababishwa na kutohaririwa kwa sababu ya waandishi kutokuwa na ujuzi wa kutosha wa uhariri. Kwa kuwa makosa mengine husababishwa na ukosefu wa uhariri au uhariri usio makini, basi suluhisho la makosa hayo ni kufanyika kwa uhariri, tena kwa umakini. Kuhusu umuhimu wa uhariri katika vyombo vya habari, Massamba (1995:8 - 9) anasema:

> Lakini ili mambo hayo au habari hiyo iweze kuwa katika lugha fasaha uhariri makini ni jambo la lazima sana. Ni juu ya mhariri kuamua ni msamiati upi unafaa, ni istilahi zipi zinafaa, ni nahau zipi zinafaa, ni tungo zipi zinafaa, n.k. Kusema kweli mhariri ndiye anayeipa ladha habari iliyoandikwa na anaweza pia kusaidia kuiundia habari sura na hisia zinazofaa.

Dondoo hili linaonesha namna uhariri unavyohitajika katika vyombo vya habari. Kuhariri kunasaidia kupunguza makosa ya lugha yanayotokea wakati wa habari na kutoa matangazo mengine. Hivyo, ni sahihi kusema kuwa, mojawapo ya suluhisho la makosa ya lugha kwenye vyombo vya habari nchini Tanzania ni kujikita katika kufanya uhariri wa kina. Hali hiyo itaongeza ufasaha wa lugha katika utoaji wa habari.

Hadi kufikia hapa, makala hii imeweza kuwasilisha na kujadili data za kipengele cha pili kinachohusu utatuzi wa makosa ya lugha yanayofanyika katika vyombo vya habari vya Tanzania ambapo umahususi uliwekwa kwenye televisheni za *TBC1, ITV* na *STAR TV*.

**Hitimisho**

Makala hii imejadili makosa ya lugha na utatuzi wake kwenye vyombo vya habari nchini Tanzania. Matokeo yameonesha kuwa wanahabari hufanya makosa mbalimbali ya lugha ambayo huathiri ufasaha wa Kiswahili. Pia, makala imewasilisha mapendekezo ya utatuzi wa makosa hayo ambayo ni kutolewa kwa mafunzo ya lugha, kuajiri wataalamu wa lugha, kuhimiza matumizi ya Kiswahili fasaha kwenye vyombo vya habari, kufanya uhariri makini na kutungwa kwa sheria za matumizi ya lugha. Hata hivyo, makala inasisitiza kuwa bado zinahitajika tafiti zingine za kuchunguza makosa mbalimbali ya lugha na utatuzi wake kwenye vyombo vya habari nchini Tanzania ili kuimarisha na kustawisha lugha ya Kiswahili, si tu katika tasnia ya habari, bali hata kwenye nyanja zingine ambazo lugha hii hutumika.

**Marejeleo**

Adaku, N.G. (2016). *Grammatical Error Analysis of Selected News Scripts of the Broadcasting Corporation of Abia State Radio, Umuahia*. (M.A Thesis) University of Nigeria, Nigeria.

Aditya, P.D., & Amita, D. (2017).Linguistic Divergences in Newspaper's Headlines. *International Journal of Engineering Technology Science and Research,* 4 (7), 858 - 864.

Akbari, E., & Kheirabadi, R. (2015). A Linguistic Analysis of Errors in News Agencies and Websites of Iran.*Theory and Practice in Language Studies,* 5 (11), 2340 - 2347.

Aruba, B.K. (2017). *Makosa ya Kisemantiki katika Mawasiliano Andishi ya Kiswahili miongoni mwa Wanafunzi wa Shule za Upili: Mfano wa Kaunti ya Kakamega* (Tasnifu ya Uzamili, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Maasai, Mara, Kenya.

BAKITA. (2015). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*.Toleo la 1. Dar esSalaam: Longhorn Publishers.

Bukagile, G.R. (2007). *Kiswahili kwa Shule za Sekondari: Kidato cha Kwanza*: Dar es Salaam: Nyambari Nyangwine Publishers.

Corder, S.P. (1967). The Significance of Learner's Errors.*International Review of Applied Linguistics in Language Teaching,* 5 (4),161 - 170.

Gass, S. M. & Selinker, L. (2008). *Second Language Acquisition: An Introductory Course*. (3rd ed). NY: Routledge, Taylor & Francis.

Gbara, N. B. (2001). *Grammatical Errors in the Nigerian Print Media and their Effect on Audience Perception and Behaviour* (Unpublished Master's Thesis). University of Nigeria.

Hassoon, F.K. (2016). A Stylistic Analysis of Selected Newspaper's Stories. *European AcademicResearch,* IV (2), 1228 - 1247.

Jagero, J. A., Mohochi, E.S., & Indede, F. (2013). The Usage of Kiswahili in Blog Discourse and the Effect on its Development. *International Journal of Humanities and Social Science*, 3 (14), 192 - 199.

Kanuri, J.M. (1995). Jukumu la Vyombo vya Mawasiliano vya Taasisi ya Elimu. Katika S.A.K. Mlacha (mh.), *Kiswahili na Vyombo vya Habari,* 48 - 52). Dar es Salaam: TUKI.

Kihore, Y. M. (2004). Masuala ya Kisarufi katika Magazeti ya Mitaani ya Kiswahili - Tanzania. *Swahili Forum*, (XI), 107 - 119.

King'ei, K. (2000). Matatizo ya Matumizi ya Lugha katika Vyombo vya Habari: Mifano kutoka Kenya. *AAP64: Swahili Forum*, (VII), 45 - 56.

Kambaya, M. (2022). Makosa ya Matumizi ya Kiswahili Yanayofanywa Katika Idhaa. Makala iliyosomwa katika Kongamano la Idhaa za Kiswahili duniani, 14 Machi, 2022 hadi 19 Machi, 2022, Jinini Arusha.

Kothari, C.R. (2004). *Resarch Methodology: Methods and Techniques*. (2nd Edition). New Delhi: New Age International (P) Ltd., Publishers.

Maina, S. (2013). Makosa katika Kiswahili, Usahihi Wake. *Mwananchi*. Ilipakuliwa kutoka https://www.mwananchi.co.tz/kolamu/lugha-yetu/Makosa-katika-Kiswahili-usahihi-wake/1614740-1914190-11lm5jk/index.html.

______ (2014). Vyombo vya Habari Gwiji wa Kuharibu Kiswahili. *Mwananchi*. Ilipakuliwa kutoka https://www.mwananchi.co.tz/kolamu/Vyombo-vya-habari-gwiji-wa-kuharibu-Kiswahili/1607214-2349288-cp8y5vz/index.html

Makunja, G.S. (1995). Sarufi na Msamiati katika Vyombo vya Habari. Katika S.A.K. Mlacha (mh.), *Kiswahili na Vyombo vya Habari* (kur. 13 - 23). Dar es Salaam: TUKI.

Massamba, D. P. B. (1995). Kiswahili kama Lugha ya Mawasiliano. Katika S.A.K. Mlacha (mh.), *Kiswahili katika Kanda ya Afrika Mashariki: Historia, Matumizi na Sera*, 1 - 11). Dar es Salaam: TUKI.

MOMT. (2018). *Mambo ya Umiliki wa Vyombo vya Habari*. http://tanzania.mom-rsf.org.

Mozūraitytė, R. (2015*). Newspaper Style: Stylistic Features of the Headlines* (Unpublished Bachelor's Thesis), Šiauliai University.

Mugambi, A., Mukuthuria, M., & Kobia, J.M. (2016a). Error Analysis in Mass Media in Kenya: A Case Study of Radio News Bulletins from Kenya Broadcasting Corporation Kiswahili Station and Radio Citizen*. International Journal of Business, Social Sciences and Education,* 2 (3), 173 - 188.

_______ (2016b). Lexical Errors in Radio News Bulletin in Kenya: A Case Study of Kenya Broadcasting Corporation Kiswahili Radio Station and Radio Citizen. *International Journal of Current Research*, 8 (04), 3023 - 3027.

Mugambi, A. (2019). The Effects of Errors from Radio News Bulletin on Communication in Selected Audiences in Kenya. *International Journal of Research and Innovation in Social Science,* III (VI), 481 - 485.

Mukhono, S. G. (2008). *Uarifu katika Taarifa za Habari: Mtazamo wa*

*Isimu Amilifu,* (Tasinifu Uzamili, haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Mukhwana, A. S., & Mukhwana, C. S. (2017).The Role of Kenya's Taifa LeoNewspaperin Enhancing Learners' Abilities in Kiswahili Language Proficience. *International Journal of Humanities Social Sciences and Education,* 4 (12), 53 - 61.

Mwansoko, H.J.M. (1995). Dhima ya Vyombo vya Habari katika Ukuzaji, Usanifishaji na Uenezaji wa Istilahi. Katika S.A.K. Mlacha (mh.), *Kiswahili na Vyombo vya Habari*, 1 - 12. Dar es Salaam: TUKI.

Mwaura, P. (2015). Mistakes and Typos are Unacceptable, But We Need to See Them in Perspective. *Daily Nation*. Ilipakuliwa kutoka https://www.nation.co.ke/oped/ opinion/Mistakes-and-typos-are-unacceptable/440808-2674442-48wmbrz/ index.html.

Odeo, I.I. & Geoffrey, M. (2008). *Fani ya Isimujamii: Kwa Shule za Sekondari*. Nairobi: Oxford University Press.

Omoera, O. S. (2008a) Linguistic Gaffes in the Nigerian Media Newscast: An Exploratory Discourse.*EJOTMAS: Ekpoma Journal of Theatre and Media Arts,* 2 (1 - 2), 62 - 77.

_______ (2008b). Miscommunication in the Nigerian Print Media: An Analysis *Ayigba Journal of Arts and Humanities*, 3.1.

Ontieri, J.O. (2015). Athari za Kifonolojia za Lugha ya Kwanza katika Kiswahili: Mfano wa Lugha Teule za Kibantu Nchini Kenya.*Mulika*, 34, 1 - 13.

Onyango, J. O. & Odawo, M.A. (2016). Kiswahili kama Chombo cha Kutangaza na KuuziaVyombo vya Habari nchini Kenya. *Mulika*, 35, 87 - 97.

Ponella, C. (1995). Matumizi ya Kiswahili katika Kanda ya Nchi Zinazotumia Kiswahili. Katika S.A.K. Mlacha (mh.), *Kiswahili katika Kanda ya Afrika Mashariki* (kur.53-57). Dar es Salaam: TUKI.

Ponera, A.S. (2019). *Misingi ya Utafiti wa Kitaamuli na Uandishi wa Tasinifu* (Tol.1). Dodoma: Central Tanganyika Press.

Rowan, K.E. (2003). Informing and Explaining Skills: Theory and Research on Informative Communication. In J.O. Greene & B. R. Burleson (eds.), *Handbook of Communication and Social Interaction Skills* (pp.403-438). New Jersey: Lawrence Erlbaum Associates Publishers.

Sewangi, S. (2017). Matatizo ya Ufasaha katika Matumizi ya Kiswahili Sanifu. *Habarileo*. Ilipakuliwa kutoka https://habarileo.co.tz/habari/matatizo-ya-ufasaha-katika-matumizi-ya-kiswahili-sanifu.aspx.

Shoo, G. (2004). Nafasi ya Kiswahili katika Vyombo vya Habari Wakati Huu wa Utandawazi. Katika BAKITA (wah.), *Kiswahili na Utandawazi* (kur. 79 - 87). Dar es Salaam: BAKITA.

Sigalla, O. (2019, 12 Julai). Vyanzo vya Upotoshaji Lugha katika Uandishi. *Habarileo,* uk.11.

Simba, J.A. (1995). Umuhimu wa Kuwa na Sera katika Idhaa za Kiswahili. Katika S.A.K. Mlacha (mh.). *Kiswahili katika Kanda ya Afrika Mashariki: Historia, Matumizi na Sera* (kur. 58-65). Dar es Salaam: TUKI.

TATAKI. (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (Tol.3). Dar es Salaam: Oxford University Press.

Telg, R. (2015). News Writing for Television and Radio.*Department of Agricultural Education and Communication, UF/IFAS Extension.* http://edis.ifas.ufl.edu.

van Dijk, T.A. (1988). News Analysis: Case Studies of International News in the Press. Hillsdale, New Jersey: Lawrence Erlbaum Associates Publishers.